WAPO WALIOLALA, KWA WENGINE...

KUMEKUCHA!

JUZUU 1 TOLEO 3

AUGUSTI 22, 2011

MWAMKO MPYA WA KIFIKRA

MIAKA 50 YA UHURU

TRIPOLI YAANGUKA

Na M. M. Mwanakijiji

Ndani ya masaa 72 Jiji la Tripoli nchini Libya limeanguka mikononi mwa waasi ambao walikuwa wanaendesha kampeni ya kumuondoa rais wa nchi hiyo Dikteta Muammar Gaddafi.

Kuanguka kwa jiji la Tripoli kunaashiria kuhitimishwa kwa kampeni hiyo iliyozidi kwa miezi sita kamili sasa na ambayo imegharimu maisha ya mamia ya wananchi wa Libya ambao wamekuwa chini ya utawala wa Gaddafi na familia yake kwa zaidi ya miaka 40 sasa. (Uk. 2)



Maelfu ya wananchi wa Benghazi, mji wa Pili kwa ukubwa wa Libya wakishangilia kuanguka kwa Tripoli kuamkia J'tatu

FIKRA PEVU

JAMII FORUMS
WHERE WE DARE TO TALK OPENLY

TANGAZA HAPA



PPF YATIMUA WANAODHANIWA KUFI-CHUA UFISADI KUPITIA JAMIIFORUMS!

Na. Mwandishi Wetu

Shirika la Pensheni la Mashirika ya Umma (PPF) limewaachisha kazi wafanyakazi watatu likiwatuhumu kuvujisha habari za ufisadi mkubwa ndani ya shirika hilo kupitia mtandao nambari moja wa habari na majadiliano wa JamiiForusm.com (Kijarida cha "Kumekucha" kinahusiana na JF). Habari ambazo kijarida chako ukipendacho kimezipata zinadokeza kuwa watumishi watatu wa shirika hilo akiwemo aliyewahi kuwa Mhasibu Mkuu Bw. Kedron




Mbwilo ambaye alihusika na kukataa kuidhinisha malipo ya



M. M. Mwanakijiji
Mhariri

SERIKALI YAHAHA KUOKOA MKATABA WA UDA NA SIMON GROUP

Mwishoni mwa juma waasi wa Libya walikuwa wanalizunguka jiji hilo la Afrika ya Kaskazini kama fundo la kamba na pole pole waliteka maeneo mbalimbali na kuzima majaribio yoyote ya utetezi wa wapiganaji wa Gaddafi. Kusika siku ya Jumamosi jioni kuamkia Jumapili waasi walikuwa kilomita chache kutoka Viwanja vya Kijani ambapo wiki kadha wa kadha mashabiki wa Gaddafi walikuwa wakikutana kutiana shime.



Maelfu ya wananchi wa Libya wakipepea bendera ya waasi - ambayo ni bendera ya zamani ya Mfalme wa Libya - walianza kujitokeza barabarani kuwapokea waasi hao na usiku wa kuamkia Jumatatu hii maelfu zaidi wamejitokeza katika mitaa na viunga vya Jiji la Tripoli kuwakaribisha waasi hao ambao wanapigana chini ya uongozi wa Baraza la Mpito la Libya ambalo linawakilisha serikali mbadala ya ile ya Gaddafi. Hadi hivi sasa nchi 32 zimetambua baraza hilo kuwa mwakilishi halali wa wananchi wa Libya. Tanzania siyo mojawapo.

Kuanguka kwa jiji hilo kuliharakishwa usiku wa Jumamosi ambapo katika hali inayoonekana kupangwa mapema misikiti ya Jiji la Tripoli ilianza kurusha matangazo ya kuwataka wananchi wa Libya kujitokeza kupigana kumuondoa Gaddafi. Wito huo unasadikiwa kuwa ulikuwa ishara kwa vikosi vya waasi wa Libya ambavyo vilikuwa vimeshaingia jijini hapo na kujipanga na silaha na kujificha kusubiri muda muafaka. Vikosi hivyo vilibadilisha mwelekeo wa vita hivyo vya wenyewe kwa wenyewe nchini Libya kwani kabla majeshi ya Libya hayajua ni wapi pa kuwazuia waasi wasiingie Libya ilijikuta tayari ina waasi katikati yake.

Pamoja na jitihada za kukatisha tamaa wapiganaji na watu wengi kwa kuwahikikishia kuwa hali ni "shwari" uongozi wa Libya ulijikuta unazidiwa. Kufika Jumapili usiku watoto watatu wa kiume wa Kanali Gaddafi walikuwa wamekamatwa na kushikiliwa mikononi na vikosi vya waasi hao.

Miongoni mwa watoto hao ni pamoja na ambaye alionekana kama msemaji mkuu wa familia Bw. Seif Gaddafi pamoja na ndugu yake Al-Saad Gaddafi. Kukamatwa kwa vijana hao ambao hawakuweza kutoa upinzani wowote kunaashiria tu kuwa walikuwa tayari kuona watu wengine wanapigania maisha yao huku wao wenyewe wakishindwa kunyanyua bunduki zao. Kukamatwa kwa watoto hao wa kiongozi huo kwaweza kuwa funzo kwa watoto wa marais wengine duniani ambao wamekuwa wakijiingiza katika utendaji kazi wa wazazi wao na kujijengea wingu la ujiko na utisho.

Mtiririko wa matukio yaliyochangia kuanguka kwa utawala wa Gaddafi tangu kuanza kwa kampeni hiyo uko hivi:

Januari 14, 2011 - Rais wa Tunisia Ben Ali anang'olewa kufuatia maandamano ambayo yamejulikana kama Machipuo ya Waarabu na kuanzisha wimbi la maandamano katika nchi kadha wa kadha za Waarabu.

Februari 11, 2011 - Rais Hosni Mubarak wa Misri naye analazimishwa kujiuzulu kufuatia maandamano na mgomo mkubwa wa wananchi kwenye viwanja wa Tahrir jijini Cairo.

Februari 15, 2011 - Wananchi wa jiji la Benghazi Mashariki ya Libya waanza maandamano ya kumpinga Gaddafi. Muda si mrefu baadaye uasi wa kijeshi unaanza na jiji la Bengazi linaangukia mikononi mwa waasi kwa urahisi, Mji wa Mistrata nao waangukia mikononi mwa waasi muda si mrefu baadaye.

Machi 15, 2011 - Vikosi vya serikali ya Libya vinafanikiwa kurudisha nyuma vikosi vya waasi na kukomboa miji karibu yote isipokuwa Mistrata na Benghazi.

Machi 17, 2011 - Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linatoa ruhusa kwa nchi wanachama kutoa msaada kuzuia mauaji ya wananchi pamoja na kuzuia ndege za Libya kuruka.

Machi 30, 2011 Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Libya Bw. Musa Kusa anaenda Uingereza na huko anaomba hifadhi ya kisiasa na kukataa kuwa mwakilishi wa Gaddafi.

Aprili 14, 2011 Viongozi wa mataifa ya Magharibi Barack Obama, David Cameron na Nicolas Sarkozy wanasema wazi "Gaddafi lazima aondoke, aondoke moja kwa moja".

Aprili 19, 2011 Baada ya waasi kufanya vibaya katika kampeni yao ya kwanza kuelekea Tripoli, maafisa wa Kijeshi toka Uingereza wanaingia Bengazi na kutoa ushauri wa kijeshi kwa waasi.

Mei 28, 2011 Vikosi vya NATO vinashambulia makazi ya Gaddafi pamoja na makao makuu ya Kamandi yake ya Kijeshi. Gaddafi ananusurika.

Juni 27, 2011 Mahakama ya Kimataifa ya The Hague, yatoa hati za kuwakamata Gaddafi na watoto wake pamoja na viongozi wengine wa juu kwa mashtaka ya uhalifu dhidi ya binadamu na makosa ya kivita.

Julai 20, 2011 Marekani yatambua rasmi Baraza la Mpito la Libya kuwa mwakilishi halali wa wananchi wa Libya.

Julai 27, 2011 Uingereza yatambua rasmi Baraza la Taifa la Mpito kuwa ni serikali halali ya Libya.

Julai 28, 2011, Kamanda Mkuu wa vikosi vya waasi wa Libya Abdel Fattah Yunus anauawa katika mazingira yaliyojaa utata.

KARIBU JAMIIFORUMS.COM

TRIPOLI YAANGUKA

Msaidizi wake ateuliwa kuongozi waasi.

Augusti 15, 2011 Waasi waanza kampeni kutoka pande zote kuelekea Tripoli. Miji ya Zawiya na Ghariyan yaangukia mikononi mwa waasi.

Augusti 20, 2011 Risasi zinaanza kusikika jiji la Tripoli baada ya vikosi vya waasi vilivyokuwa vimeshatangulia na kujificha (sleeper cells) vilipoanza kujitokeza.

Augusti 21, 2011 Waasi waingia katikati ya jiji la Tripoli, watoto wawili wa Gaddafi watekwa na mmoja (Mohammed) ajisalimisha mwenyewe.

Hata hivyo, kuanguka kwa Tripoli hakujakamilika hadi kijarida hiki kinatoka. Rais wa Libya haijulikani alipo japo kuna tetesi kuwa amekimbia nchi lakini kuna uwezekano yeye naye anaweza kuangukia kwenye mikono ya waasi. Kuanguka kwa Tripoli hata hivyo hakumaanishi kuwa mgogoro wa kisiasa utakuwa umefikia kikomo. Kama kilichotokea Misri ni mfano, basi Libya inakazi kubwa ya kuanza kujenga taasisi za kiutawala.

Wakati huohuo Rais wa Syria Bw. Bashar Al Assad amehakikishia wananchi wake kuwa serikali yake haiko katika hatari ya kuanguka kufuatia maandamano ambayo kama yale ya Libya yalianzishwa na matukio ya Tunisia miezi karibu saba nyuma. Hata kama Gaddafi, Assad aliamua naye kuzima uasi kwa kutumia vikosi vya jeshi. L Pamoja na matumizi makali ya nguvu dhidi ya wananchi wake bado wananchi wa Syria wameendelea kujitokeza kupinga utawala wake.
Wananchi wa Libya wanasubiria kwa hamu kusikia hatima ya Kanali Gaddafi.

Serikali ya Tanzania ambayo imepokea misaada mingi toka kwa Gaddafi haijaonesha ujasiri wa kutambua Baraza la Taifa la Libya na haijajulikana kama itakuja kufanya hivyo.

PPF YATIMUA WANAOSHUKIWA KUFICHUA UFISADI

zaidi ya shilingi bilioni 1 kwa watu sita katika mfumo na mtindo ambao umetiliwa mashaka na watu mbalimbali.

Maafisa wengine ni pamoja na Bw. Siriel Mchembe ambaye alikuwa ni Meneja wa michango pamoja na Bw. Emmanuel Kakuyu ambaye alikuwa ni Kaimu Mkurugeni Mkuu ambaye alidaiwa kugongana na Mkurugenzi wa shirika hilo Bw. William Erio (Pichani). Bw. Erio ni mpwa wa Rais wa zamani Bw. Benjamin William Mkapa ambaye ndiye alimteua kwenye nafasi hiyo wiki chache kabla ya kuondoka madarakani mwaka 2005.

Maelezo yaliyotolewa na uongozi huo kwa watumishi huo ni madai ambayo yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza kuwa watumishi hao "imethibitishwa" kuwa walihusika na kutoa taarifa mbalimbali za shirika hilo kwenye mtandao wa JamiiForums na kwa kufanya hivyo kuonekana kuwa wanatishia wanachama wapya wasijiunge na PPF na vile vile kudaiwa kuhamasisha wanachama wengine wajitoe kwenye mfuko huo.

Hata hivyo vyanzo vyetu mbalimbali vimezidi kudokeza kuwa wahusika halisi wa sakata hilo siyo hao waliotajwa au kufukuzwa kazi kwani wafanyakazi wengi na watumishi wa ngazi za juu wa shirika hilo wanatambua kiini na kina cha ufisadi huo mkubwa.

Kuanzia mwaka jana na hatimaye mwaka huu vyombo vya habari mbalimbali vilidokeza juu ya ufisadi mkubwa uliofanyika. Miongoni mwa mambo ambayo yamefunuliwa wazi ni jinsi uongozi wa juu wa shirika hilo ukiongozwa na Bw. William Erio ulijigawia fedha za "shukrani" pamoja na "pensheni" kwa kiasi kisichopungua shilingi milioni 200 kwa kila mmoja japo ya kwamba wote walikuwa wamefanya kazi kwa miaka mitatu.

Pamoja na ufisadi huo ni madai ya kiasi cha zaidi ya shilingi nusu bilioni ambazo Bw. Erio anadaiwa kujichotea kwa kisingizio cha "mkataba" na "kustahili". Taarifa tulizonazo zinaonesha kuwa Bw. Erio peke yake alilipwa shilingi milioni 520 pamoja malipo mengine ambayo ni shukrani sawa na asilimia 25 ya ya mishahara yake yote ambayo ilikuw sawa na karibu shilingi milioni 150, shukrani ya utumishi wa muda mrefu, shilingi milioni 11 pamoja na asilimia 40 ya mishahara yake ya miezi 12 sawa na shilingi milioni 75. Hiyo pia ikamuweka sawa kuanza mkataba mpya na hakuna kiongozi yeyote Bungeni ambaye amekuwa na ujasiri wa kupigia kelele.

Malipo haya na mtindo huu unawakumbusha watu kashfa ya malipo ya namna hiyo kwa aliyekuwa Mkurugenzi mkuu wa Wakala wa Barabara wa Tanzania (TANROADS) Bw. Ephraim Mrema. Kilichowavuruga watu kwenye sakata la Mrema ni jinsi mkataba wake alioingia ulimuwekea marupurupu manono na kumpa nguvu ambazo baadhi ya watu waliamini kuwa hazikuwa halali.

Hata hivyo sakata la PPF limeonekana kuwa gumu kwa viongozi wakubwa serikali kulishughulikia kutokana na uzito wake na hasa uhusiano wake na Rais Mkapa pamoja na vigogo wengine ambao wanandugu kwenye mfuko huo. Hata baadhi ya wakuu wa vyombo vya usalama nao wana jamaa katika ngazi za juu za mfuko huo kiasi kwamba imekuwa vigumu kwa taasisi huru kuweza kufanya uchunguzl huru.

Kufukuzwa kwa watumishi hao kunaashiria kampeni ya vitisho kwa watumishi wa umma ambao watajitokeza kufichua ufisadi kwenye taasisi za umma. Serikali ya Tanzania na hasa Bunge lake limekuwa gumu kutunga sheria ya kuwalinda wanaofichua ufisadi (whistleblower protection act) na matokeo yake kama tukio hili kiliachiliwa - kama inavyotarajiwa - itakuwa mwanzo wa kusababisha watumishi waadilifu kuanza kufumbia macho maovu katika idara na taasisi zao kwa kuogopa kisasi (retaliation).

Vyanzo vyetu halisi ndani ya shirika hilo hata hivyo vimeahidi kutokukata tamaa wala kutishwa kwani kinachogombaniwa ni haki na utu wa watumishi wote na siyo kikundi cha watu wachache. "Sisi tutaendelea kufichua ufisadi, kwani haiwezekani watu waliofanya kazi miaka mitatu tu walipwe mabilioni wakati wazee wetu na watumishi waliotumikia nchi hii kwa miaka kumi kadhaa walipwe pensheni za shilingi elfu hamsini, sabini au hata laki moja" alisema mmoja wa vyanzo vyetu kwa masharti ya kutokutajwa jina lake.

Mitandao ya kijamii imekuwa sauti huru kwa Watanzania ambao wameamua kujitoea mhanga kufichua ufisadi na kulazimisha kuwajibika. Kutokana na hili mitandao yetu yote ambayo tunashirikiana nayo imeanza kuongeza na kutilia mkazo usiri wa wanachama wake ili kuweza kuwasaidia watu kutembelea mitandao hiyo pasipo hofu.

Soma bure

WAPO WALIOLALA, KWA WENGINE...

PICHA YA WIKI



Makamu wa Rais Dr. Bilal akiwa na Rais Mstaafu A. H. Mwinyi pamoja na washirika wa mashindano ya kuhifadhi Qurani yaliyofanyika mwishoni mwa Juma Dar. (Picha na VPO)

Katuni ya wiki



KUHUSU 'KUMEKUCHA'

Kijarida cha Kumekucha hutolewa mara kwa mara kwa kushirikiana na mtandao wa Jamiiforums.com. Ni kijarida huru zaidi cha habari za kisiasa na kitaifa ambacho kina lengo la kuamsha fikra za Watanzania kudai mabadiliko yenye manufaa kwao Kwani Watanzania wanastahili zaidi ya wanavyopata sasa!

Unaweza kuunga mkono JamiiForums.com na "Kumekucha". Wasiliana na:

Support@jamiiforums.com
au
Mwanakijiji@jamiiforums.com

Donate now with..
PayPal

Pamoja na habari za matukio mbalimbali "Kumekucha" itakuletea makala fupi za hoja kutoka kwa waandishi, wanasiasa na wanaharakati mbalimbali. Ili makala yako ifikiriwe kutoka kwenye kijarida chako kipya ukipendacho, tuandikie "mwanakijiji@jamiiforums.com". Makala yake iwe katika lugha ya kiswahili au Kiingereza na ISIZIDI ukurasa mmoja.

MAKTABA YA MIAKA 50 YA UHURU



Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere akiwa na Nelson Mandela na Winnie jijini Dar

KUMEKUCHA

Mchapishaji

B. G. M Production
Timu ya Waandishi
M. M. Mwanakijiji – Mhariri

Freddy Katunzi–Habari za Siasa

Mahmoud Rashid–Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mwanakijiji@jamiiforums.com

Tovuti: http://www.jamiiforums.com

Kanusho: *Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki. Habari zote ni kwa ajili ya burudani na kuelimishana. Jithibitishie kila usomalo.*